

**102/3**  
**KISWAHILI**  
**FASIHI**  
**JULAI/AGOSTI-2014**  
**MUDA : Saa 2 $\frac{1}{2}$**

## **MTIHANI WA TATHMINI YA PAMOJA YA KAUNTI NDOGO RACHUONYO KUSINI**

*Hati ya Kuhitimu Elimu ya Sekondari Kenya. (K.C.S.E)*

**102/3**  
**Kiswahili**  
**Fasihi**  
**Saa : 2 $\frac{1}{2}$**

### **MAAGIZO:**

- 1) Jibu maswal **Manne** pekee.
- 2) Swali la **kwanza** ni la **Lazima**.
- 3) Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nnez ilizobaki, yaani; Tamthilia, Ushairi,Riwaya na Fasihisimulizi.
- 4) Usijibu maswali **Mawili** kutoka **Sehemu moja**.
- 5) Maswali yote yajibiwe kwa lugha ya Kiswahili

*Karatasi hii inakurasa **4** zilizopigwa chapa. Watahiniwa ni lazima waangalie kama kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.*

**SEHEMU YA A : HADITHI FUPI**  
**DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE.**

***Swali la lazima***

1. Ndoa ni asasi inayokumbwa na changamoto kadhaa katika Jamii ya leo. Jadili ukweli wa kauli hii kwa kurejelea hadithi zifuatazo :  
(a) Mke wangu  
(b) Maeko  
(c) Mwana wa Darubini  
(d) Maskini Babu yangu

**SEHEMU YA B : TAMTHILIA**  
**MSTAHIKI MEYA: Timothy Arege.**

***Jibu swali la 2 au la 3***

2. Tamthilia ya **Mstahiki Meya** inasawiri Picha halisi ya mataifa mengi barani Afrika. Dhihirisha. (al.20)
3. “Wakisubiri ugonjwa nao utasubiri ? ”  
(a) Fafanua muktadha wa dondo hili. (al. 4)  
(b) Tambua kwa kutolea mifano tamathali mbili za usemi zinazojitokeza katika dondo hili. (al. 4)  
(c) Eleza sifa na umuhiu wa mzungumzaji katika dondo hili. (al.12)

**SEHEMU YA C : RIWAYA**  
**KIDAGAA KIMEMWOZEA: Ken Walibora**

***Jibu swali la 4 au la 5***

4. Asasi ya ndoa katika riwaya ya **Kidagaa Kimemwozea** inakabiliwa na changamoto nyingi fafanua. (al. 20)
5. “Ndio, Mtu hujikuna ajipatapo. Sina hela za nauli wala za chumba cha kulala”  
(a) Eleza muktadha wa maneno haya. (ala. 4)  
(b) Ni masaibu gani mengine yaliyomkumba msemaji wa maneno haya ? (ala. 10)  
(c) Fafanua sifa zozote **nne** za msemewa. (al. 4)  
(d) Eleza maudhui yanayojitokeza katika dondo hili (ala. 2)

**SEHEMU YA D : FASIHI SIMULIZI**

6. (a)Maigizo ni nini ? ( ala. 2)  
(b) Eleza aina **mbili** kuu za maigizo (al. 2)  
(c) Eleza sifa zozote **nne** za maigizo ( al.8)  
(d) Fafanua majukumu ya tamasha za maigizo nchini Kenya. (ala. 8)

**SEHEMU YA E : USHAIRI**

7. *Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuatia.*

1. Sina ni kukosekana, si kuwa ni ubahili,  
Watu hutarajiana, kupana zao fadhili,  
Kiwapo chapatikana, chenye kuzidi shughuli,  
Sina si kuwa bahili, sina ni kukosekana.

2. Iwapo mwenzio hana, cha ziada kukujali,  
Ndipo anenapo sina, kukuafu yako hali,  
Usidhani ni hiyana, chake kuwa hakubali,  
Sina si kuwa bahili, sina ni kukosekana.
3. Yapasa kukumbukana, tuishipo mbali mbali,  
Kila mtu jambo yuna, limtialo thakili,  
Akawa ni mwenye dhana, la kesho kulikabili,  
Sina si kuwa bahili, sina ni kukosekana.
4. Na pindi anapoona, tarehe mno i mbali,  
Na katika muawana, punje ya rasilimali,  
Nyumbani kiwa hakuna, kukupa rntu muhali,  
Sina si kuwa bahili, sina ni kukosekana.
5. Kutaka ungekazana, nasaha na tafadhali.  
Endapo hana namna. mwenzio lile na hili  
Bora ni kuombeana, Mungu awape sahali  
Sina si kuwa bahili, sina ni kukosekana.
6. Wajua watu hupana, kiasi cha kuhimili,  
Mioyo kukunjuana, imani kuwa kamili.  
Akwambaye leo sina, kesho kweli takujali,  
Sina si kuwa bahili, sina ni kukosekana.
7. Hasa munaopendana. pendo lisotamthili,  
Kichache na zaidana. furahani na madhili  
Daima mwaambatana. leo ni gani ajili,  
Sina si kuwa babili, sina ni kukosekana.

### ***Maswali***

1. Lipe shairi hili kichwa mwafaka. (al. 2)
2. Taja na ueleze bahari **mbili** zinazojitokeza katika shairi hili. (al.4)
3. Eleza umbo la shairi hili. (al. 4)
4. Andika ubeti wa 6 kwa lugha nathari (ala.4)
5. Taja mifano **mitatu** ya maneno ambayo yameandikwa kishairi na kisha uyandike kisanifu. (al. 3)
6. Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivtotumiwa katika shairi
  - (a) Bahili (al 1)
  - (b) Fadhili (al.1)
  - (c) Thakili (al.1)

### **8. Soma shairi kisha ujibu maswali yanayoufua tia.**

Mgomba umelala chini hauna faida tena  
 Baada ya kukatwa na kufanya kazi  
 Wa bustani kwa kusita  
 Watoto, kwa wasi wasi ~~wanasubiri~~ wakati wao  
 Watoto hakuna kitu  
 Isipokuwa upepo fulani wenyewe huzuni  
 Unaotikisa majani na kutoa sauti ya kilio

Hivyo ndivyo ufalme wa mitara uliyivo  
Mti ya mji umelala chini hauna faida tena  
 Baada ya kukatwa na wafanyakazi  
 Wa bustani kwa kusita  
 Chumbani hakuna kitu  
 Isipokuwa upepo fulani wenyewe huzuni utingishao  
 Wenyewe hila waliozunguka kitanda na kulia  
 Machozi yenyewe Matumaini ya piga.  
 Mbiu ya hatari ya magomvi nyumbani.  
 M ago mvi  
 Kati ya wanawake  
 Magomvi  
 Kati ya watoto kwa ajili ya vitu na uongozi  
 Ole! Milki ya ‘Lexanda imekwisha!

#### Vidonda nya ukoma visofunika

Ambavyo kwa muda mrefu vilifichana  
 Sasa viko nje kufyonzwa nzi kila aina  
 Na vinanuka vibaya  
 Lakini inzi kila mara hufyonza wakifikiri  
 Nani watamwambukiza.

#### ***Maswali***

- a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka (al. 2)
- b) Taja wahusika wanaojitokeza katika shairi (al.2)
- c) Yataje mambo **manne** yanayotendeka baada ya mgomba kuka twa (al.4)
- d) Tambua sifa zozote **nne** zinazokifanya kifungu hiki kuwa shairi. (al. 4)
- e) Onyesha kwa tafsiri mbinu ya lugha ya uandishi katika shairi hili ukiondoa mifano mwafaka (al. 4)
- f) Andika methali **tatu** zinazoweza kurejelewa katika shairi hili. (al.3)
- g) Kwa kutolea mifano taja na ufanue mbinu **mbili** za Uhuru wa ushairi katika shairi hili (al. 4)
- h) Eleza maana ya mafungu yafuatayo yaliyotumiwa kama mafumbo katika shairi (al.2)
  - i) Vidonda nya ukoma
  - ii) Mti ya mji umelala chini